**KIAMBATANISHO A**

**TAARIFA YA MAENDELEO YA BARAZA LA BIASHARA WILAYA YA MPWAPWA KUANZIA 2015-2018**

| DBC MEETING DATE (TAREHE YA MKUTANO WA BARAZA) | AGENDA OF THE MEETING (AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA) | RESOLUTIONS PASSED (MAAZIMIO YALIPITISHWA NA KIKAO) | ACTION TAKEN ON RESOLUTIONS TO DATE (UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO HADI SASA) | CHALLENGES ON WORKING ON RESOLUTIONS (CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO) |
|---|---|---|---|---|
| 18/04/2015 | KUKUSANYA MAONI TOKA KWA WANANCHI KUHUSU KUBORESHA RASIMU YA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI | KILIUNDWA KIKOSI KAZI KILICHOUNGANISHA SEKTA BINAFSI NA SEKTA YA UMMA ILI KUZUNGUKA KATIKA KILA KATA KUKUSANYA MAONI | KIKOSI KAZI KILIKUSANYA MAONI NA KUWASILISHA KATIKA BARAZA, BARAZA LILICHAMBUA NA KUFANYA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO. KWASASA SHERIA NDOGO IMESAHINIWA NA WAZIRI MUHUSIKA, IMEPIGWA CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI NA KUTANGAZA KATIKA GAZETI LA SERIKALI NA KUANZIA TAREHE 01/07/2017 IMEANZA KUTUMIKA | HAKUNA |
| 09/09/2015 | UPATIKANAJI WA HATI ZA KIMILA | WAJUMBE WALIAZIMIA AFISA ARDHI NA MALIASILI AANDAE TARIFA INAYOONYESHA UPATIKANAJI WA HATI | JUMLA YA HATI ZA KIMILA 650 ZIMETOLEWA KWA UFADHILI WA MKURABITA KWA ENEO LA PWAGA | UKOSEFU WA FEDHA ZA UPIMAJI NA UANDAAJI WA HATI |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | MILIKI ZA VIWANJA NA MASHAMBA NA CHANGAMOTO ZAKE NA KUWASILISHA KATIKA KIKAO KIJACHO | | |
| | UKOSEFU WA VIWANDA VYA KUSAFISHA NA KUFUNGASHIA MAFUTA YA ALIZETI PAMOJA NA KUSINDIKA KARANGA | WAJUMBE WALIAZIMIA AFISA KILIMO,UMWAGILIAJI NA USHIRIKA AANDAE TAARIFA YENYE TAKWIMU INAYOONYESHA UZALISHAJI WA MAZAO YA KARANGA,ALIZETI NA UFUTA KWA MIAKA MITATU(3) ILIYOPITA NA KUIWASILISHA KATIKA KIKAO | TAARIFA ILIWASILISHWA NA KWA MUJIBU WA TAFITI ZILIZOFANYWA NA LIC ZILIONYESHA KUWA TATIZO SIO UKOSEFU WA VIWANDA ILA NI UZALISHAJI MCHACHE WA ALIZETI, HIVYO WAKULIMA WAHAMASISHWE KUONGEZA NGUVU KATIKA KILIMO. | HAKUNA |
| | MAPENDEKEZO YA SKIMU ZA UMWAGILIAJI | WAJUMBE WALIAZIMIA KUUNDA KIKOSI KAZI KITAKACHOANDIKA ANDIKO KUHUSU UCHIMBAJI WA MABWA NA UKARABATI WA MIFEREJI YA UMWAGILIAJI NA KUIWASILISHA KATIKA KIKAO KIJACHO. | KIKOSI KAZI KIMEANDIKA NA KUTAJA MAENEO AMBAYO YAFANYIWE UPEMBUZI YAKINIFU NA WATAALAMU ILI KUONA ENEO LIPI LINAFAA KUJENGWA MABWAWA NA MIFEREJI. | HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14/05/ 2016 | KONGANO LA UTALII | WAJUMBE WALIKUBALIANA NA WAZO LA KUANZISHA UTALII KATIKA WILAYA NA KUUNDA KIKOSI KAZI KWAAJILI YA KUVITAMBUA VIVUTIO VYOTE VYA UTALII VILIVYOPO WILAYANI MPWAPWA. | KIKOSI KAZI KILIWASILISHA KAZI HIYO KATIKA KIKAO CHA BARAZA LA BIASHARA KILICHOFANYIKA TAREHE 31/03/2017. WAJUMBE WALIPOKEA TAARIFA NA KUKIAGIZA KIKOSI KAZI KUFANYA MAREKEBISHO YA TAARIFA YAO HASA KATIKA PICHA NA MAELEZO YA VIVUTIO. | HAKUNA |
| | UFAHAMU JUU YA TOZO MBALIMBALI TOKA MAMLAKA YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI (TFDA). | MAMLAKA ILIALIKWA KUTOA MAFUNZO YA TOZO MBALIMBALI. | WAJUMBE WALIAZIMIA MAMLAKA IWE INATOA MAFUNZO HAYO MARA KWA MARA KWA WAFANYABIASHARA. | HAKUNA |
| | UPIMAJI UDONGO KWA AJILI YA KILIMO WILAYANI MPWAPWA. | WAJUMBE WALIPOKEA WAZO NA KUIAGIZA OFISI YA KILIMO KUTUMA TAARIFA HIYO NA KUOMBA KUWEZESHWA LIC. | LIC WALIPOKEA MAOMBI NA KUIAGIZA OFISI YA KILIMO KUCHAGUA MAENEO(VIJIJI) VICHACHE VYA KUANZIA VIPIMO HIVYO.<br><br>MPAKA SASA OFISI YA KILIMO TAYARI IMEKWISHA REKEBISHA ANDIKO KWA KUCHAGUA | HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | KIJIJI CHA MAFAU, KITATI, MALOLO, MATOMONDO NA WOTTA, NA ANDIKO LIMETUMWA LIC. | |
| 20/08/2016 | | | | |
| | UJENZI WA KIWANDA CHA KUCHAKATA NGOZI | WAJUMBE WALIPOKEA TAARIFA NA KUTOA USHAURI WA VIKUNDI HIVYO VIWILI KUUNGANA KWA KUWA KAZI NA MALENGO YAO YANAFANANA. | MPAKA SASA VIKUNDI HAVIKO TAYARI KUUNGANA NA KURUDISHA TAARIFA KWA MCHAKATO ZAIDI | VIKUNDI KUTOKUWA TAYARI KUUNGANA |
| | MFUMO WA KUKUSANYIA MAPATO YA HALMASHAURI. | WAJUMBE WALIPOKEA TAARIFA NA KUISHAURI HALMASHAURI KUANZA KUTUMIA MFUMO HUO ILI HALMASHAURI IWEZE KUONGEZA MAPATO YAKE. | HALMASHAURI INAENDELEA KUKUSANYA MAPATO YAKE VIZURI KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELECTRONIC. | HAKUNA |
| 23/11/2016 | MPANGO WA KUONDOA VIWANDA VIDOGOVIDOGO KATIKA MAKAZI YA WATU MPWAPWA MJINI. | WAJUMBE WALIAZIMIA LITAFUTWE ENEO NA KUFANYIWA TAHIMINI IKIWA NI PAMOJA NA KUANGALIA MIUNDOMBINU YA UMEME NA MAJI. | ENEO LIMEPATIKANA AMBALO NI ENEO LA VISELE, LIMEPIMWA, RAMANI IMEANDALIWA NA KUPELEKWA WIZARA YA VIWANDA, MPAKA SASA RAMANI IMEPITISHWA NA ENEO KURUHUSIWA KUTUMIKA KWA MATUMIZI YA VIWANDA. AIDHA KATIKA KIKAO CHA TAREHE 08/01/2018 WAJUMBE WALISHAURI MAMLAKA YA MAJI NA UMEME IANZE KUPELEKA HUDUMA HIZO MUHIMU ILA KUWEZA KUWAVUTIA | ENEO BADO HALIJALIPWA FIDIA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | MPANGO KAZI PAMOJA NA BAJETI VIANDALIWE NA KUWASILISHWA KATIKA KIKAO. | WAFANYABIASHARA. MPANGO KAZI ULIWASILISHWA KATIKA KIKAO | |
| | UCHAGUZI WA TOZO MOJA KATI YA USHURU WA HUDUMA NA USHURUWA HOTELI | WAJUMBE WALICHAGUA USHURU WA HOTELI UONDOLEWE UBAKI WA HUDUMA. | TAARIFA YA UCHAGUZI WA TOZO ULIPELEKWA TAMISEMI.<br><br>KWA SASA USHURU WA HUDUMA UMEANZA KULIPWA KUANZIA TAREHE 01/07/2017 | HAKUNA |
| | MREJESHO WA MAANDIKO | ANDIKO LA UPEMBUZI YAKINIFU KWA MAENEO YANAYOFAA KUJENGWA MABWAWA MAJIBU NI KWAMBA LIC WAMETOA MAELEKEZO YA NAMNA YA KUREKEBISHA ANDIKO, KWA SASA ANDIKO LIMEREKEBISHWA NA KUTUMWA LIC.<br><br>KUHUSU UJENZI WA SOKO LA MJIMPYA, WAJUMBE WALIAZIMIA KUWE NA RATIBA MAALUM NA MPANGO KAZI WA UJENZI WA SOKO LA MJIMPYA. | TUNASUBIRI MAJIBU KUTOKA LIC<br><br>AGIZO LILIZINGATIWA AMBAPO HADI SASA IMEUNDWA KAMATI YA KUSIMAMIA UJENZI KWA MFUMO WA PPP (USHIRIKIANO KATI YA SEKTA YA UMMA NA | HAKUNA<br><br>HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | SEKTA BINAFSI) NA KAZI YA UKAMILISHAJI WA SOKO INAENDELEA,KIASI CHA SHS 14,000,000 KIMEPOKELEWA KWA AJILI YA SHUGHULI HIYO NA HADI SASA KAZI YA CHOO UNAENDELEA NA MPANGO KAZI UMEAMBATANISHWA. | HAKUNA |
| | | KUHUSU MRADI WA KUWAWEZESHA WAKULIMA WADOGOWADOGO KUPATA MBEGU BORA YA NGURUWE KUTOKA CHUO CHA KILIMO NA MIFUGO VISELE-WAJUMBE WALIAZIMIA KUWA VISELE IANDAE MPANGO KAZI NA KUWASILISHA KATIKA KIAKO KINACHOFUATA PIA LIC ITOE TAARIFA YA KIASI CHA FEDHA AMBACHO KIMESHATOLEWA. | CHUO CHA VISELE KIMEWASILISHA MPANGO KAZI NA LIC WAMEWASILISHA KWA MAANDISHI KIASI KILICHOTOLEWA KWA AJILI YA MRADI HUO. | MRADI HAUKUFANIKIWA KWA KUWA NGURUWE WALIPATWA NA UGONJWA NA KUFARIKI |
| | | UJENZI WA MNADA WA ILOLO—WAJUMBE HAWAKURIDHIKA NA MAJIBU HIVYO WALIOMBA UFAFANUZI ZAIDI KUTOKA LIC | TAARIFA ILIWASILISHWA LIC, KWA SASA TUNASUBIRI MAJIBU KUTOKA LIC. | HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | KUHUSU UPIMAJI WA UDONGO KWA AJILI YA KILIMO—LIC WALISHAURI IDARA YA KILIMO ICHAGUE MAENEO MACHACHE YAKUANZA NAYO. IDARA ILICHAGUA KIJIJI CHA MAFUA, KITATI, MALOLO, MATOMONDO NA WOTTA NA KUTOA TAARIFA LIC. | TUNASUBIRI MAJIBU KUTOKA LIC | HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 31/03/ 2017 | UJENZI WA VITUO VYA BODABODA MPWAPWA MJINI. | WAJUMBE WALIAZIMIA KIKOSI KAZI KIUNDWE NA KUFANYA KAZI ZIFUATAZO;<br>➢ KUTEMBELEA MAENEO YOTE YALIYOPENDEKEZWA KWA AJILI YA KUTHIBITISHA UMUHIMU WA UWEPO WA KITUO KATIKA ENEO HUSIKA.<br>➢ KUANDAA MICHORO (DESIGN) YA VIBANDA<br>➢ KUANDAA BAJETI YA UJENZI | KIKOSI KAZI KIMESHAFANYA TAHIMINI NA TAARIFA ILIWASILISHWA KATIKA KIKAO CHA KAMATI TENDAJI.<br>KWA SASA MHANDISI UJENZI ANAENDELEA KUFANYA MAREKEBISHO YA GHARAMA ZA UJENZI ILI TAARIFA | HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | WA VITUO HIVYO.<br>➢ KUANDAA MPANGO KAZI WA UJENZI WA VITUO HIVYO.<br>➢ KUWASILISHA TAARIFA KATIKA KIKAO | IWASILISHWE KATIKA BARAZA LA BIASHARA NA KUTUMWA LIC. | |
| | UJENZI WA SOKO LA MAZAO | SOKO LA MAZAO LIJUMUISHWE KATIKA RAMANI YA KITUO CHA BIASHARA (COMMERCIAL HUB) ITAKAYO ANZISHWA ENEO LA ISIGHU | WATAALAMU BADO WANAENDELEA NA KAZI YA KUANDAA RAMANI HUSIKIA. | HAKUNA |
| | MAWASILISHO YA BAJETI YA BARAZA LA BIASHARA KWA MWAKA 2017 | WAJUMBE WALISHAURI KUWA HALMASHAURI PAMOJA NA SEKTA BINAFSI IJIPANGE KATIKA KUONGEZA UACHANGIAJI | USHAURI UMEPOKELEWA | SEKTA BINAFSI HAINA CHANZO MAHUSUSI CHA KIPATO ILI KUWEZA KUONGEZA UCHANGIAJI WA KUENDESHA BARAZA, HIVYO KWA SASA WANAJIANDAA KUONA NAMNA GANI WANAWEZA KUPATA CHANZO CHA KIPATO ILI WAWEZE KUCHANGIA VYEMA SHUGHULI ZA BARAZA. |
| | MAWASILISHO YA TOVUTI YA HALMASHAURI | WAJUMBE WALISHAURI KUWA TOVUTI IWE INAENDA NA WAKATI NA MATUKIO(UPDATE) | USHAURI UNAFANYIWA KAZI | UKOSEFU WA VIFAA VYA KUKUSANYIA HABARI KAMA LAPTOP NA CAMERA. |
| 08/01/2018 | TAARIFA KUHUSU BARAZA LA BIASHARA(kuanzishwa ,muundo,mwongozo,majukumu,vikao vya kisheria) | MAFUNZO YATOLEWE KWA WAJUMBE ILI WAJUMBE WAWE NA UWEZO WA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO VYEMA | AGIZO LIMEZINGATIWA NA MAFUNZO KWA WAJUMBE WA SEKTA BINAFSI YALIFANYIKA TAREHE 23/01/2018 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI. PIA MAFUNZO KWA WAJUMBE WA SEKTA YA UMMA | HAKUNA |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | YATAFANYIKA TAREHE 09/02/2018 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI. | |
| | MREJESHO WA CHANGAMOTO MBALIMBALI ZILIZOWASILISHWA NA SEKTA BINAFSI BAADA YA ZIARA YA WAJUMBE WA SEKTA BINAFSI BARAZA LA BIASHARA KATKA KATA 16 ZA WILAYANI MPWAPWA | WAKUU WA IDARA KWA KUSHIRIKIANA NA WATENDAJI WENGINE WAWEKE MAJIBU ANA USHAURI WALIOWASILISHA KATIKA SURA YA KIUTENDAJI | AGIZO LIMEZINGATIWA NA UTEKELEZAJI UNAENDELEA. | HAKUNA |